ewura

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji

ISO 9001: 2015 Certified

HALIUZWI

Newsletter

SEPT 2020

ISSN 1821 - 7273 TOLEO NA. 28

OMCs wathibitisha uwepo wa mafuta Uchaguzi Mkuu

Kauli Mbiu: *"Udhibiti wa Haki kwa Matokeo CHANYA - IMPACT"*

Toleo Lililopita

BODI YA WAHARIRI

MWENYEKITI
Mha. Godfrey H. Chibulunje

MHARIRI
Bw. Titus M. Kaguo

MHARIRI MSAIDIZI
Bw. Wilfred Mwakalosi

WAANDISHI
Bi. Asiatu Msuya
Bi. Tobietha Makafu

MAKAO MAKUU YA EWURA,
Jengo la EWURA,
Kiwanja Na 3, Kitalu AD,
S.L.P. 2857, Dodoma,
Simu: +255 26 2329002-4,
Nukushi: +255 26 2329005,
Barua pepe: info@ewura.go.tz;
Tovuti https://www.ewura.go.tz
Simu ya BURE 0800110030

Mitandao ya Kijamii

Facebook: https://www.facebook.com/ewuranews
Twitter: https://www.twitter.com/ewuratanzania
You Tube: EWURA TV

YALIYOMO

Kutoka kwa Mhariri 3
OMCs wathibitisha uwepo wa mafuta Uchaguzi Mkuu. 4
Katibu Mkuu Maji aipongeza EWURA kwa kazi nzuri... 5
Biashara ya petroli, gesi ya kupikia zazidi kukua 6
NPGIS: Mfumo wa kidikitali wa upatikanaji wa taarifa za mafuta na gesi asilia..... 7
Mfumo wa kulinda njia za miundombinu waja 8
EWURA yafanikisha kutatua migogoro Kanda ya Kasikazini..... 9
Mafundi umeme wenye leseni za EWURA Singida wakaguliwa 10
Mkuu wa Wilaya kutoa elimu ya Mkataba wa Huduma kwa Wateja 11
Mamlaka za maji zafundishwa ufuatiliaji wa ubora wa maji..... 12
Ewura yang'ara Maonesho ya Sabasaba, Nane Nane. 13
Ripoti ya mwaka yaonesha utendaji wa EWURA upo kileleni..... 14

PICHA KUU:

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Mhandisi Godfrey Chibulunje (wa pili kushoto) akiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Total Tanzania, Bw. Jean-Francois Schoepp (katikati) katika picha ya pamoja na Mkurugenzi wa Petroli wa EWURA, Bw. Gerald Maganga (kulia), Mkuu wa Masuala ya Sheria wa Total Tanzania, Bi. Marsha Msuya (wa pili kulia) na Meneja wa Biashara wa Petroli wa EWURA, Bi. Kemi Kafanabo (kushoto), baada ya kumaliza mazungumzo na Mhandisi Chibulunje alipotembelea wafanyabiashara wa mafuta kwa ujumla (OMCs) ili kujiridhisha juu ya kuwapo kwa mafuta katika Uchaguzi Mkuu ujao.

KUTOKA KWA MHARIRI

Wapenzi Wasomaji wetu!

Titus M. Kaguo

Ninawakaribisha wote kujiunga nasi katika toleo jipya la Jarida la Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), toleo la 28 katika mfululizo wa machapisho ya majarida ya EWURA kwa mwaka 2020.

Kwa heshima na taadhima napenda kukualika kusoma habari za kuvutia kutoka katika shughuli mbalimbali za udhibiti zilizotekelezwa na EWURA katika kipindi cha robo mwaka cha kati ya Julai na Septemba 2020. Jarida la EWURA, mara zote huchapisha taarifa za shughuli za udhibiti zilizofanyika katika kipindi cha robo mwaka husika na kwa toleo hili, linabeba habari za shughuli za kiudhibiti zilizotekelezwa katika kipindi cha Julai hadi Septemba 2020.

EWURA inadhibiti sekta ndogo tatu za nishati ambazo ni Petroli; Umeme na Gesi Asilia na Sekta moja ya Maji; Maji na Usafi wa Mazingira.

Katika kipindi hiki, EWURA imetekeleza shughuli mbalimbali za kiudhibiti ambazo baadhi zake, zimechapishwa katika toleo hili, ambalo linachapishwa katika kutekeleza maagizo ya Sheria ya EWURA Sura na 414 ya Sheria za Tanzania, kipengele cha 6(e).

Kipengele cha 6(e) kinasema kwamba ni wajibu wa Mamlaka kuhakikisha inaboresha ustawi wa jamii ya Watanzania kwa kuimarisha elimu kwa umma, ufahamu na uelewa wa sekta zinazodhibitiwa ikiwa ni pamoja na; haki na wajibu wa walaji na watoa huduma wa sekta zinazodhibitiwa; Njia za kutatua migogoro na kusikiliza malalamiko, kazi na shughuli za mamlaka kwa ujumla.

Katika toleo hili pamoja na mambo mengine, habari zilizochapishwa ni pamoja na wafanyabiashara wa mafuta kwa ujumla kuwahakikishia Watanzania kuwepo kwa mafuta muda wote wakati wa Uchaguzi Mkuu; unazishwaji wa mfumo mpya wa taarifa katika mkondo wa juu, kati na chini wa shughuli za mafuta na EWURA kuibuka mshindi wa tatu katika maonesho mbalimbali; na habari nyingi za kuvutia zaidi.

Karibuni!

OMCs wathibitisha uwepo wa mafuta Uchaguzi Mkuu

Titus Kaguo na Kemi Kafanabo

Kampuni za Uuzaji wa Mafuta za TANZANIA (OMCs) zimeihakikishia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) usalama thabiti wa usambazaji wa bidhaa za petroli wakati wa shughuli za Uchaguzi Mkuu wa 2020.

Akizungumza kwa nyakati tofauti wakati wa ziara zilizofanywa kwa makampuni hayo -OMCs, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Mhandisi Godfrey Chibulunje alihakikishiwa na Watendaji Wakuu wa Jumla wa Total Tanzania, GBP Tanzania na Oryx Energy kuwa watasambaza bidhaa za petroli za kutosha wakati na baada ya kipindi cha Uchaguzi Mkuu.

Wakati wa ziara hizo, ambazo Mkurugenzi wa Petroli, Bw. Gerald Maganga na Meneja Biashara wa Petroli, Bi. Kemi Kafanabo aliandamana na Eng. Chibulunje, OMCs walisema wako tayari kufanya kazi kwa masaa mengi ili kuhakikisha usambazaji wa bidhaa za petroli unakuwa sawa kote nchini.

Wakati nchi inaelekea kwenye Uchaguzi Mkuu, matumizi halisi ya mafuta ya kila siku ya dizeli katika robo ya tatu ya mwaka 2020 ilifikia lita milioni 5.83 ikiongezeka kutoka lita milioni 5.14 zilizopatikana mwaka 2019; na ile ya petroli imefikia lita milioni 4.61 ikiongezeka kutoka lita milioni 3.654 zilizopatikana mwaka 2019.

Wakati wa ziara hizo, Eng. Chibulunje alipokea maoni kadhaa yaliyokusudiwa kuboresha usalama wa usambazaji wa bidhaa za mafuta.

OMCs waliibua wasiwasi wa waendeshaji wengine wasio waaminifu kuuza bidhaa kwa punguzo kubwa ambalo ni chini ya gharama ya bidhaa na kusababisha upotezaji wa biashara kwa waendeshaji wenye ufanisi.
Pendekezo liliwasilishwa kwa EWURA kuanzisha bei kikomo ya chini ili kuhakikisha Mamlaka inalinda wasambazaji wenye ufanisi kama vile bei inayotolewa kila mwezi inavyolinda watumiaji. Mhandisi Chibulunje alisema EWURA na Mamlaka zingine zinazohusika ikiwa ni pamoja na Tume ya Ushindani wanalichukua suala hilo ili lichambuliwe.

Masu ala mengine ambayo yalizungumziwa ni pamoja na mikataba ya usambazaji wa mafuta ambayo wauzaji wanahitaji kuingia na wauzaji wa jumla, kufikia 30 Septemba 2020 na taarifa kwa umma za hivi karibuni zilizotolewa na EWURA zinazohitaji kwamba wauzaji wanaofanya kazi katika mikoa ya Kaskazini na Kusini kuchukua bidhaa kutoka bandari za Tanga na Mtwara.

Mhandisi Chibulunje alisisitiza juu ya lengo la Serikali, pamoja na mengine, kuhakikisha usalama wa usambazaji nchini kwa kutumia bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara. Kampuni hizo ziliarifiwa kwamba zinapaswa kuagiza bidhaa za petroli kupitia bandari ya Tanga kuwahudumia wateja wao wa mikoa ya Kaskazini na kupitia bandari ya Mtwara kuwahudumia wale wa mikoa ya Kusini.

Katibu Mkuu Maji aipongeza EWURA kwa kazi nzuri

Na Tobietha Makafu

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga, ameipongeza Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), kwa kusimamia vizuri majukumu ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji nchini.

Amesema ingawa bado kumekuwa na changamoto mbalimbali, huduma zimeendelea kupatikana kwa wakati na kwa bei halisi.

Katibu Mkuu huyo alitoa pongezi hizo alipofanya ziara ya kikazi katika Ofisi za EWURA makao makuu, mkoani Dodoma hivi karibuni na kuzungumza na menejimenti kuhusu utekelezaji wa majukumu na mafanikio yake.

Akiwasilisha mada juu ya mafanikio ya taasisi yake, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA ,Mhandisi Godfrey Chibulunje alisema, EWURA imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa weledi, ambapo hata baada ya kutokea mlipuko wa ugonjwa wa Covid 19, huduma ziliendelea kupatikana kote nchini.

Mhandisi Chibulunje alitaja baadhi ya mafanikio yaliyopatikana kuwa ni pamoja na kuongezeka kwa idadi ya leseni za vituo vya mafuta, leseni za mafundi umeme, kupanda madaraja kwa baadhi ya mamlaka za maji na kuongezeka kwa matumizi ya gesi asilia hasa katika viwanda na kwa baadhi ya magari.

Akizungumzia sekta ya maji, Mhandisi Sanga aliipongeza EWURA kwa kusimamia mamlaka za maji nchini na kuziwezesha kujitengenezea mipango ya biashara inayosaidia kufanya kazi kwa weledi na kuongeza tija katika kuhakikisha huduma ya maji inakuwa bora.

“Nawapongeza sana, mmesimamia utengenezaji wa mipango ya biashara kwa mamlaka za maji nchini, hivyo niwaombe tena muongeze nguvu katika kuhakikisha mipango ya biashara hio, inaendeana na mipango mikakati wanayojiwekea ili kufikia malengo katika kutoa huduma ya maji safi na usafi wa mazingira” alisema Mhandisi Sanga.

Mhandisi Chibulunje aliahidi kuwa EWURA itaendelea kuweka mizania ya maslahi sawa kati ya wadau husika, hivyo kuchochea ongezeko la tija, ushindani, na upatikanaji wa huduma bora kwa wote. Pia itaendelea kuzingatia misingi mikuu sita ya utawala bora katika maamuzi ya udhibiti ambayo ni weledi, uwajibikaji, utabirikaji, ushirikishaji, uwazi na kufuata Sheria.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga (katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Menejimenti ya EWURA alipotembelea Makao Makuu ya EWURA.

Biashara ya petroli, gesi ya kupikia zazidi kukua

Na Wilfred Mwakalosi

Soko la ndani la bidhaa za petroli na gesi ya kupikia (LPG) limeendelea kukua kwa kasi, kutokana na mazingira na usimamizi mzuri wa sekta hii unaofanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA).

Kufikia Desemba 2019, idadi ya vituo vya Mafuta vinanvyofanya kazi ilifikia 1,596, ikiwa imepanda kutoka vituo 1,460 kwa mwaka uliotagulia, saw ana ongezeko la asilimia 9.32, taarifa ya utendaji wa sekta iliyotolewa na mdhibiti hivi karibuni imeeleza.

“Kuongezeka kwa vituo vya mafuta kumechangiwa na kuongezeka kwa mahitaji, ongezeko la shughuli za kiuchumi na ongezeko la mtandao wa barabara,” imeeleza taarifa hiyo. Hata hivyo, vituo vingi vimejengwa maeneo ya kwenye miji, ingawa kuna ongezeko kubwa la mahitaji ya mafuta maeneo ya vijijini.

Mkurugenzi wa Idara ya Petroli EWURA, Bw. Gerald Maganga, alisema hivi karibuni kwamba mdhibiti ameendelea kuhamasisha ujenzi wa vituo vya mafuta vijijini ili kuhakikisha bidhaa hiyo inapatikana maeneo hayo kwa uhakika na usalama.

“Kwa sababu hii, kanuni za uuzaji rejareja wa mafuta maeneo ya vijijini za mwaka 2017 zitaendelea kutumika, ambapo baadhi ya mahitaji kwa ajili ya kibali cha ujenzi wa kituo kwa maeneo hayo yamepunguzwa ili kupunguza gharama za uwekezaji bila kuathiri masuala ya afya, usalama na uhifadhi wa mazingira,” alisema.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, usalama wa upatikanaji mafuta nchini umeendelea kuwa wa uhakika. Kwa wastani, kampuni za mafuta zimekuwa na mafuta ya kutosha kwa matumizi ya nchi kwa siku zaidi ya 20, ikiwa ni juu ya mahitaji ya siku 15 kama inavyotakiwa kisheria.

Jumla ya lita bilioni 6.1 za mafuta (dizeli, petroli, mafuta ya taa, mafuta ya ndege na mafuta mazito ya mitambo HFO) ziliingizwa nchini mwaka 2019, ikiwa ni ongezeko la asilimia 7 ikilinganishwa na bidhaa zilizoingizwa mwaka 2018.

Kati ya bidhaa hizo, asilimia 57 zilikuwa kwa ajili soko la ndani na zilizobaki zilikwenda nchi jirani za Zambia, Congo (DRC), Rwanda, Malawi na Burundi.

Mafuta yaliyoingizwa nchini kwa ajili ya matumizi ya soko la ndani mwaka 2019 yalikuwa lita 3. 5 bilioni, ambalo ni ongezeko la asilimia 8.4 ikilinganishwa na lita 3. 2 bilioni za mwaka uliotangulia.

Ongezeko hilo lilichangiwa na miradi mingi ya serikali inayoendelea, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa barabara, reli ya SGR na bwawa la kufua umeme la Mwalimu Nyerere. Vile vile, mafuta yamekuwa yanatumika kwenye sekta ya kilimo ambako shughuli zake zimezidi kuongezeka hasa kwa sababu ya uwepo wa mvua za kutosha.

Biashara ya gesi ya kupikia nayo imeendelea kukua kwa kasi, kwa kuwa na ongeeko la gesi iliyoingia nchini na vitega uchumi vipya. Mwaka 2019, jumla ya tani 166,436 za LPG ziliingizwa nchini, ikilinganishwa na tani 142,939 zilizoingizwa mwaka 2018, ikiwa ni ongezeko la asilimia 16.

Asilimia 65 ya gesi iliyoingizwa nchini ilikuwa kwa ajili ya matumizi ya ndani, wakati asilimia 35 ilisafirishwa kwenye masoko ya nje, ambapo asilimia 70 ilikwenda Kenya.

Ongezeko la gesi iliyoingizwa nchini linatokana na juhudi za serikali na makampuni ya gesi kuhamasisha wananchi kutumia nishati hiyo dhidi ya mkaa na kuni.

Kwa mujibu wa Bw. Maganga, licha ya ongezeko la matumizi ya LPG nchini, kuna usambazaji usiokidhi mahitaji maeneo ya vijijini. “jitihada Zaidi zinahitajika kwa wasambazaji wa gesi ya LPG kupanua mtandao na kuwafikia wenye kipato cha chini ili waweze kupata nishati hii ya LPG,” alisema.

NPGIS: Mfumo wa kidikitali wa upatikanaji wa taarifa za mafuta na gesi asilia

Na Asiatu Msuya

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imeanzisha mfumo wa kitaifa wa kidijitali wa ukusanyaji, uratibu na uunganishaji wa taarifa za shughuli za mkondo wa juu, wa kati na wa chini wa sekta ya petroli na gesi asilia.

Mfumo huo unaojukana kama NPGIS ambao huwezesha kupata taarifa za kila siku, kila wiki na kila mwezi na kutoa ripoti anuwai za masuala ya mafuta na gesi asilia nchini, utaihudumia EWURA, Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), Wizara ya Nishati, Wizara ya Fedha, Taasisi ya Taifa ya Takwimu na taasisi zote za Serikali za kimkakati.

Akieleza dhumuni la kuanzishwa kwa mfumo huo, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Mhandisi Godfrey Chibulunje alisema NPGIS ni kitovu cha kukusanya na kuchangamanisha taarifa kwa pamoja za masula ya petroli na gesi asilia nchini; na inawezesha kupata takwimu sahihi kwa utekelezaji na ufanisi wa shughuli za kiudhibiti na ukusanyaji mapato ya Serikali.

Mkurugenzi wa Petroli wa EWURA, Bw.Gerald Maganga kwa upande wake, alieleza kuwa, kupitia NPGIS, EWURA itapata kwa urahisi taarifa za makisio ya mahitaji ya mafuta, uingizaji wa mafuta kwa aina, wingi, bei na chanzo; taarifa za kutolewa kwa mafuta melini kwenda ghalani, ikiwa ni pamoja na jina la chombo, aina za bidhaa na muda wa kutoka. Pia mfomu huo utatasaidia kutambua akiba ya mafuta kwa aina na wingi katika milki ya wauzaji; mauzo na matumizi; pamoja na mambo mengine.

EWURA inatoa mwito kwa wadau wote kushirikiana katika kuhakikisha mfumo huo, ambao pia utaunganishwa na mifumo mingine ya Serikali, unakuwa na tija kwa kuwasilisha taarifa husika kwa wakati, kwani si tu utainufaisha EWURA, bali wadau wote wa sekta ya mafuta na gesi asilia nchini.

Mfumo wa kulinda njia za miundombinu waja

Na Wilfred Mwakalosi

Mamlaka ya udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ipo kwenye hatua za mwisho kukamilisha mpango utakaosaidia kupambana na uwezekano wa majanga kutokea kwenye njia za wazi inakopita miundombinu ya huduma mbalimbali kama gesi, maji na umeme.

Mpango huo utahusisha utunzi wa sheria na kanuni za kudhibiti miundombinu chini ya ardhi hasa wakati wadau wanapofanya matengenezo, marekebisho au ujenzi utakaohusisha uchimbaji kwenye maeneo yenye miundombinu.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Mhandisi Godfrey Chibulunje alisema tayari hati ya makubaliano ya kuwawezesha wadau wa miundombinu kuandaa mpango wa pamoja wa kulinda miundombinu hiyo imesainiwa na wadau hao hivi karibuni.

“Baada ya hati hiyo ya makubaliano kusainiwa, kamati ya ufundi ya pamoja itaundwa, ili kutengeneza kanuni za kisheria zinazoendana na makubaliano hayo, na EWURA itakuwa inafuatilia wadau namna wanavyofuata kanuni, taratibu na miongozo, jambo ambalo litasiaidia Mamlaka kutoa haki kwenye usuluhishi wa migogoro,’ alisema.

Hati ya makubaliano itasaidia kuongeza usalama wa umma na mali zao, uadilifu na umadhubuti wa mfumo wa miundombinu ya ardhini, kwa kuanzisha na kutumia mbinu za kisasa za kuzuia uharibifu wa miundombinu nchini kote.

Taasisi zinazotegemewa kusaini hati hiyo ya makubaliano ni kampuni ya simu (TTCL), Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira (DAWASA), Pan African Energy (PAET), SONGAS, na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC).

Nyingine ni shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), kampuni ya gesi ya Maurel & Prom, Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA), Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) na Kampuni ya Bomba la Mafuta (TAZAMA Pipelines Limited).

“EWURA, TPDC na PAET mwaka 2018 zilijadili na kukubaliana kuchukua hatua za haraka kushirikisha wadau wote—wamiliki wa njia hizo na watumiaji—ili kutafuta namna ya kuwa na mfumo utakodhibiti usalama wa miundombinu wakati wa ukarabati, matengenezo, marekebisho na ujenzi unaohusisha uchimbaji,” alisema Kaimu Mkurugenzi huyo.

Kwa mujibu wa mtendaji mkuu huyo, miaka ya hivi karibuni imeshuhudia ongezeko la ajali zinazotokana na kukosekana kwa udhibiti wa njia za miundombinu zinazotumiwa na wadau wengi.
Kwa mujibu wa taarifa, matukio hayo ni pamoja na ajali ya Aprili 2014 iliyotoea Kurasini Darajani, ambapo kampuni ya China Railway Construction Engineering Group (CRCEG) ilitoboa bomba la gesi wakati ikiendelea na shughuli zake.

Mwezi Mei 2014, kampuni ya Shalom Engineering ilitoboa bomba la gesi eneo la Kurasini jirani na TEC, wakati katika tukio linguine, Januari 2018, DAWASCO ilitoboa bomba la gesi eneo la Buguruni kwa Mnyamani na kusababisha moto mkubwa.

Mwezi Septemba, 2018 wajenzi wa reli ya Standard Gauge (Yapi Merkezi) walisababisha uharibifu kwenye bomba la gesi eneo la Ilala Bungoni jijini Dar es Salaam.

Katika juhudi za kutafuta suluhisho la kudumu la tatizo la usalama wa miundombinu hii, EWURA kwa kushirikiana na Jumuia ya wadhibiti wa Marekani (NARUC) na Shirika la misaada ya kimataifa la Marekani (USAID) walikutana mwaka 2018 na kuitisha kikao kujadili uzito wa tatizo la usalama wa miundombinu na na jinsi ya kukabiliana nalo.

Kikao hicho kilipitisha azimio kwamba EWURA iongoze uundwaji wa hati ya makubaliano ili upatikane mfumo wa kutatua changamoto hizo. Kila taasisi itatoa wawakilishi wawili ili kuunda kamati ya ufundi kwa mujibu wa sehemu ya tatu ya hati ya makubaliano. Kamati hiyo ya ufundi baadaye itaanza kutengeneza kanuni na miongozo.

EWURA yafanikisha kutatua migogoro Kanda ya Kasikazini

Na Evelyn Shundi

Wakazi wa Kata za Ekenywa, Mula na Olturoto wilayani Arusha wamefanikiwa kupata muafaka wa malalamiko yao dhidi Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), kwa kuwekewa mashine umba (Transformer) ambayo imeongeza nguvu ya upatikanaji wa umeme katika maeneo hayo na hivyo kumaliza kabisa kero iliyokua inawakabili ya umeme mdogo.

Pia mkoani Kilimanjaro, eneo la Rau Msufini, Kata ya Mabogini wilaya ya Moshi vijijini waliokua na malalamiko ya miundombinu chakavu ya usambazaji umeme wameweza kufanyiwa maboresho na TANESCO kwa kuwekewa miundombinu mipya ya nguzo, nyaya na mashine umba (transformer).

Mkazi wa eneo hilo, Bw. Khalifa Mwinyimkuu, ameishukuru EWURA kwa kushughulikia na kumaliza changamoto hiyo ya miundombinu chakavu iliyokua inahatarisha mali na maisha ya wakazi wa eneo la Rau Msufini. Aidha, wateja mbalimbali waliokua na malalamiko ya ankara sizizoakisi uhalisia wa matumizi, kusitishiwa huduma kinyume na taratibu, kucheleshwa kuunganishiwa huduma, kuuziwa au kununua bidhaa za petroli zisizo na ubora katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Tanga yamepatiwa ufumbuzi katika kipindi cha mwaka 2019/2020.

Pia, wateja wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira katika mikoa ya Arusha, Kiliamanjaro na Tanga wamepatiwa suluhu ya malalamiko yao ya ankara sizizoakisi uhalisia wa matumizi, kusitishiwa huduma kinyume na taratibu, kucheleshwa kuunganishiwa huduma.

Katika kushughulikia migogoro na malalamiko ya wateja dhidi ya watoa huduma ama ya watoa huduma dhidi ya wateja, EWURA huzingatia kanuni na taratibu ili kuhakikisha mteja anatimiza wajibu wake wa kulipia huduma kwa wakati, kutunza, kulinda miundombinu ya huduma na mtoa huduma anatoa huduma bora inayozingatia afya, usalama na mazingira.

Malalamiko hayo yanaweza kuwasilishwa kwa njia ya barua, nukushi; barua pepe info@ewura.go.tz; au kupitia mfumo wa kieletroniki ujulikanao kama LOIS unaopatikana katika tovuti ya EWURA https://lois.ewura.go.tz. Aidha, Baraza la Watumiaji wa Huduma zinazodhibitiwa na EWURA (EWURA CCC) linaweza kuwasilisha malalamiko mahususi au malalamiko yanayogusa watu wengi. Pia, kikundi cha watu kinaweza kuwasilisha malalamiko, kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa Kanuni za Taratibu za Kutatua Migogoro G.N.10/2013.

Mafundi umeme wenye leseni za EWURA Singida wakaguliwa

Na Mha. Evarist Simon

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) hivi karibuni iliendesha zoezi la kukagua kazi za mafundi umeme mkoani Singida kwa lengo la kujiridhisha na ubora wa kazi hizo, hususan endapo shughuli za ufungaji umeme zinafanywa kwa weledi na kwa mujibu wa kanuni na utaalamu kwa kuzingatia madaraja ya leseni walizopewa mafundi hao.

Ukaguzi huo ulihusisha mafundi wanaofanya kazi za ufungaji umeme majumbani, maeneo ya biashara na taasisi mbalimbali, sambamba na kusikiliza na kutatua changamoto wanazokutana nazo mafundi hao.

Ukaguzi pia ulilenga kupima uelewa wao wa Kanuni za EWURA za Ufungaji Umeme za Mwaka 2019 ambazo ni nyenzo muhimu kwenye utendaji wa kazi zao za kila siku.

Katika ukaguzi huo,EWURA ilibaini kuwepo mapungufu katika shughuli za ufungaji umeme kwa mafundi wengi kutokuwa na vitendea kazi sahihi, hivyo kujaza taarifa zisizo sahihi kwenye fomu za wateja wao na kuwasilishwa TANESCO. Pia ukaguzi huo ulibainisha mafundi hao kutokuwa na uelewa wa Kanuni za EWURA za Huduma za Umeme za Mwaka, 2019.
Ukaguzi wa miundo mbinu ya huduma za umeme ni mojawapo ya jukumu la EWURA. Ukaguzi pia huhusisha miundombinu ya TANESCO ya uzalishaji meme, usafirishaji, ugavi, uunganishaji wa umeme na ujazaji wa fomu za maombi ya umeme ya wateja ambazo hupaswa kujazwa na mafundi umeme.

Sheria ya Umeme ya Sura Namba 131 inamtaka mtu yeyote anayefanya kazi za ufungaji mifumo ya umeme nchini kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA. Kwa mantiki hiyo, fundi yeyote mwenye leseni ya EWURA anaweza kufanya kazi za umeme katika mkoa wowote kulingana na daraja la leseni yake ambalo ni A,B,C,D na W.

Ifahamike pia kuwa ni kosa kisheria kujishughulisha na kazi za umeme bila kuwa leseni iliyotolewa na EWURA na adhabu yake kwa mhusika atakayepatikana na hatia ni faini isiyopungua Shilingi milioni tano au kifungo cha miaka mitano au vyote kwa pamoja.

Mhandisi Evarist Simon (kushoto) wa EWURA akikagua Swichi Kuu (main switchboard) na fomu ya maombi ya umeme ya mteja katika mtaa wa Mitundurini, Singida. Wengine ni Omary Hamisi Mtaturu na Haruna Jumanne wote wakiwa ni mafundi umeme wenye leseni daraja C zilizotolewa na EWURA.

Mkuu wa Wilaya kutoa elimu ya Mkataba wa Huduma kwa Wateja

Na Getrude Mbiling'i

Mkuu wa wilaya ya Nzega, ACP Advera Bulimba amesema yupo tayari kutoa elimu juu ya Mkataba wa huduma kwa wateja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), baada ya kueelewa umuhimu wake kwa kupata huduma bora.

"EWURA mmenipa rungu, ninaahidi kutoa elimu kwa wananchi pindi nitakapokuwa natekeleza majukumu yangu sehemu mbalimbali za Wilaya hii ili waelewe umuhimu wa mkataba wa huduma kwa wateja kama nyenzo muhimu ya kupata huduma bora," alisema ACP Bulimba alipokuwa anazuingumza hivi karibuni na uongzozi wa EWURA Kanda ya Kati.

ACP. Bulimba, alisema wateja wengi, akiwamo yeye, hawafahamu uwepo na upatikanaji wa mkataba huo, na huenda hicho ndiyo kikwazo moja wapo cha kupata huduma bora kutoka kwa watoa huduma husika.

ACP. Bulimba alifurahishwa na elimu aliyoipata kutoka EWURA na kuahidi kushirikiana na EWURA kutoa elimu kwa wananchi pindi atakapokuwa akitekeleza majukumu yake.

Kaimu Meneja wa EWURA Kanda ya Kati, Mhandisi Maurus Martin, akielezea umuhimu wa mkataba huo alipomtembelea ACP Bulimba alisema mkataba huo umesaidia sana pande zote za wadau wa EWURA.

"Mkataba wa huduma kwa wateja unaeleza kwa kina haki na wajibu wa pande zote mbili; lengo ni kuhakikisha huduma zinatolewa kwa kufuata, sheria, kanuni na taratibu na kwa kuzingatia viwango vinavyokubalika katika utoaji wa huduma," alieleza Mhandisi Martin.

Aidha, Mhandisi Martin alifafanua kuwa, watoa huduma wote wanaodhibitiwa na EWURA, wanapaswa kuwa na mkataba wa huduma kwa mteja, na kuwa wateja wanapaswa kuiomba mikataba hiyo kwa watoa huduma wao ili waweze kufahamu namna ambavyo viwango vya huduma vinapaswa kuwa, pamoja na haki na wajibu wao katika kupata huduma hizo.

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) inao mkataba wa huduma kwa mteja ambao imekuwa ikiutumia kama moja ya nyenzo muhimu za utekelezaji shughuli zake za udhibiti.

Mkataba huo, pamoja na mambo mengine, umeanisha masuala muhimu ya kiudhibiti pamoja na muda wa kuyashughulikia masuala hayo ili kuhakikisha kunakuwepo ufanisi na tija pamoja na kuimarisha uhusiano wa kiutendaji baina ya mtoa huduma na mpokea huduma.

Mkataba wa Huduma kwa Mteja wa EWURA unapatikana katika tovuti ya Mamlaka www.ewura.go.tz.

Mkuu wa Wilaya ya Nzega, ACP Advera Bulimba (wa pili kushoto) katika picha ya pamoja na ujumbe wa EWURA Kanda ya Kati ukiongozwa na Kaimu Meneja wa EWURA Kanda ya Kati Mha. Martin Maurus (kushoto) na Ofisa Mwandamizi wa Huduma kwa Wateja Kanda ya Kati, Bi Getrude Mbiling'i (katikati) na Ofisa Mwandamizi wa Mawasiliano na Uhusiano wa EWURA Makao Makuu, Bi Asiatu Msuya wakati walipofanya ziara ya kikazi wilayani Nzega. Kulia ni Katibu Tawala wa Wilaya ya Nzega, Bw. Onesmo Kisoka.

Mamlaka za maji zafundishwa ufuatiliaji wa ubora wa maji

Na Tobietha Makafu

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imeendesha mafunzo kwa mamlaka za maji nchini, kuhusu Muongozo wa pili wa Ufuatiliaji wa Ubora wa Maji safi na Maji Taka, ili kuzifanya mamlaka hizo, kuandaa mipango ya ufuatiliaji wa ubora wa huduma ya maji safi na maji taka wanayotoa kwa wananchi.

Mwongozo huo unonesha taratibu za kufuata, katika kutekeleza mambo muhimu ya ufuatiliaji wa ubora wa majisafi na maji taka, kwa kuzingatia changamoto zinazozikumba mamlaka hizo, ili kuhakikisha kuwa huduma za majisafi na maji taka zinatolewa kwa kulinda afya na mazingira ya watumiaji.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Bw. Nzinyangwa Mchany alisema:"Mambo muhimu ya kuzingatia katika ufuatiliaji wa ubora wa majisafi na maji taka ni pamoja na kuwa na vipimo sahihi vya ubora wa majisafi na maji taka, kuwa na ratiba na idadi ya uchukuaji wa sampuli za kupimwa, kufuata kanuni na miongozo pamoja na kutoa ripoti ya ubora wa maji hayo.

Aliongeza: "Tunatumai kuwa mtatekeleza majukumu yenu kwa kuandaa mpango wa ufuatiliaji wa ubora wa usambazaji wa majisafi na majitaka. Lengo kuu ni kuhakikisha kuwa huduma mnazotoa zinakidhi vwango vya vitaifa vya vbora wa majisafi na majitaka kwa ustawi na usalama wa watumiaji."

Mwongozo huu, toleo la pili umekuja baada ya miaka mitano ya utekelezaji wa Toleo la Kwanza, kutokana mabadiliko kadhaa na changamoto zilizotokea katika kipindi hicho, ikiwa ni pamoja na mageuzi anuwai katika sekta ya maji kama vile kupitiwa upya kwa sifa za viwango vya maji vya Shirika la Viwanga Tanzania na kutungwa kwa sheria mpya za kitaifa kama Sheria ya Ugavi wa Maji na Usafi wa Mazingira (2019).

Ewura yang'ara Maonesho ya Sabasaba, Nane Nane

Na Tobietha Makafu

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imeibuka mshindi wa tatu, katika maonesho ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam, DITF (Sabasaba) na Maonesho ya Wakulima (Nanenane) yaliyofanyika kati ya mwezi wa saba na wa nane mwaka huu, katika mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya na Arusha.

Katika Maonesho ya DITF (Sabasaba), EWURA iliibuka mshindi wa tatu katika taasisi zinazotoa huduma za Nishati wakati katika maonesho ya Nane nane yaliyofanyika Kanda ya Kaskazini mkoani Arusha, iliibuka mshindi wa tatu kwa taasisi za udhibiti. Pia EWURA iliibuka mshindi wa tatu katika kundi la taasisi zinazodhibiti ubora wa huduma na viwango. katika maonesho yaliyofanyika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini mkoani Mbeya.

Akizungumza katika sherehe za kufunga maonesho ya Sabasaba tarehe 13 Julai 2020, Waziri wa Viwanda na Biashara wa Zanzibar, Balozi Amina Salumu Ally, alitoa pongezi kwa washindi wote walioshiriki maonesho hayo na kusema: "Tuzo hizo mlizopata ziwe chachu ya kuendelea kutoa huduma nzuri kwa wananchi," alisema.

Naibu Spika wa Bunge la Tanzania, Dkt Tulia Ackson (kulia), alikabidhi cheti cha ushindi wa tatu kwa Meneja wa EWURA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mhandisi Karim Ally katika maonesho ya Nane Nane yaliyofanyika mkoani Mbeya kwa ajili ya mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano EWURA, Bw. Titus Kaguo, alisema: "EWURA imedhamiria kuhakikisha elimu ya udhibiti inafika kwa kila mtumiaji wa huduma za nishati na maji".

Aliongeza kuwa kwenye maonesho EWURA hutoa ripoti za utendaji wa kila sekta, vipeperushi na kuwapatia elimu ya jinsi tunavyotatua migogoro na malalamiko, jinsi ya kuomba leseni, pamoja na kuwaelezea kazi na wajibu wa mdhibiti.

EWURA pia ilishiriki maonesho hayo katika ofisi zake zote za kanda, ikiwa ofisi ya Kanda ya Ziwa ilishiriki katika maadhimisho ya kitaifa mkoani Simiyu, Kanda ya Kati ilishiriki mkoani Dodoma na Kanda ya Mashariki ilishiriki Mkoa wa Morogoro.

Ripoti ya mwaka yaonesha utendaji wa EWURA upo kileleni

Na Tobietha Makafu

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ni taasisi iliyojipanga kutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya kiuchumi wa Taifa la Tanzania, pamoja na watu wake katika kutoa huduma za kiudhibiti.

Kwa mujibu wa Taarifa ya Mwaka ya 13 ya EWURA utendaji wa Mamlaka katika mwaka wa fedha ulioishia mwezi Juni 2019, inaelezea mafanikio na changamoto katika kipindi hicho.

Akizungumzia ripoti hiyo, aliyekuwa Kaimu Mkurugenzi wa EWURA, Bw. Nzinyangwa Mchany alisema katika mwaka wa fedha 2018/2019, EWURA ilifanikiwa kufikia viwango vya ubora wa kimataifa, katika utoaji wa huduma kwa kuhakikisha Mamlaka inafanya shughuli zake kuendana na viwango vya kimataifa.

Katika sekta ya mafuta, ripoti hiyo inaonesha kwamba utaratibu wa uagizaji wa pamoja wa bidhaa za petrol, umeendelea kuwa wa mafanikio zaidi hasa baada ya kupanuka kwa kuongeza Bandari ya Mtwara kuwa bandari ya tatu kuanza kupokea mafuta baada ya Dar es Salaam na Tanga.

Akizungumzia gesi asilia Bw. Mchany alisema Taarifa hiyo imeonesha kuwa EWURA imefanikiwa kuandaa jumla ya kanuni 8 katika kudhibiti Gesi Asili ambayo inakua kwa kasi katika miaka ya karibuni.

Katika kuchochea utendaji wa mamlaka za maji zinazodhibitiwa na EWURA, Bw. Mchany alisema, EWURA imepitia na kutoa vigezo vipya vya kutathimini madaraja ya leseni za watoa huduma za majisafi na usafi wa Mazingira na kutoa mafunzo ya uandaaji wa mipango ya biashara kwa mamlaka za wilaya na miji midogo 33.

Kwa mujibu wa Taarifa hiyo, EWURA imefanikiwa kupitia nyenzo za udhibiti na kutengeneza nyingine mpya, ambazo jumla ya nyenzo 25 zimepitiwa na kuboreshwa, 12 zikiwa za gesi asilia, 7 za umeme na 6 za petroli.

Kuhusu shughuli za utoaji wa leseni, Taarifa inaonesha kwamba jumla ya leseni 1,208 zilitolewa, ambapo leseni 544 ni za sekta ya petroli, 8 umeme, (Leseni 3 za muda, 5 za uzalishaji wa umeme), 2 za maji safi na usafi wa mazingira. Pia EWURA ilitoa leseni 654 kwa mafundi wa umeme.

Taarifa hiyo pia imeonesha mafanikio katika kutoa elimu kwa umma kwa kuendesha semina mbalimbali kuhusu kazi, wajibu na majukumu ya mamlaka, haki na wajibu wa watoa huduma na vilevile namna ya EWURA inavotatua malalamiko.